TANGAZO LA SERIKALI Na. 312 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURAYA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA NYAMIGOTA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Nyamigota ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 385333MS 9670468KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ124°MS kwa umbali wa kilomita 1.02 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji nmaba B yenye majira - nukta 386294MS, 9671081KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ133° kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 386289MS, 9671641KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ130°MG kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 386106MS, 9671810KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katiaka uelekeo wa MG126° kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 385787MS, 9671766KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ95°MG kwa umbali wa kilomita 0.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 386295MS, 9671652KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS139°MG hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 384624MS 9671598KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS131° kwa umbali wa kilomita 0.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upiamjai namba H yenye majira - nukta 384584MS, 9671401KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS96°MS kwa umbali wa kilomita 1 hadi ulipoanzia"

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*